RAIS Moi akifungua Mfereji wa Maji huku Mwanamke umoja akichota maji baada ya Rais kufungua mpango wa Maji wa Barushi, Kilifi.
PICHA: KENYA NEWS AGENCY

KIPINDI CHA TATU CHA MASOMO KINAPIGA HODI

SKULI ZOTE nchini Kenya za msingi na upili zinaingia katika kipindi cha tatu cha masomo, nacho ni kipindi cha mitihani ya mwisho wa mwaka na pia kwa madarasa mengine, ni kipindi cha kumalizia maisha ya kiskuli kwa ujumla. Kwayo ni dhahiri kwamba hichi ni kipindi muhimu sana katika maisha ya mwanafunzi, kwani kipindi hichi huja kumuamuliaa iwapo ataendelea tena na masomo ya mbele ama iwapo ulimwengu wa elimu ameshaagana nao. Kama wahenga walivyosema, "Kila aliyae hushika kichwache' nasi watu wa Wilaya ya Mombasa ama Mwamnbao wa Kenya hatuna budi kushika vichwa vyetu na tukaanza kufikiria vile ambayo vijana wetu watafanya katika mitihani yao na zile fursa watakazozipata za kujiendeleza kimasomo.

Siku ya kwanza ya kufungua shule ndiyo siku ya kufikiria namna ya kufaulu mtihani, kwani siku ya mwisho ya skuli huwa firimbi imekwishalia na fursa huwa ime yoyoma.. Tuwafikirie vijana wetu wa shule za msingi hapa Mombasa amabo mpaka dakika hii bado hawajapawa mtihani wa mazoezi wa C.P.E. Sawa ya mtihani huu, ni kufanywa wakati wa kipindi cha pili wiki za mwanzo kabisa ili kumpa nafasi mwalimu namwanafunzi kila mmoja kupima kazi yake aliyofanya na iwapo hiyo C.P.E. ataweza kuimudu. Mtihani huu watakiwa mapema ufanywe na matokeo yake yajulikane kwa kila mzazi ili apate kumrekebisha mtoto wake kwa pale ambapo bado akali dhaifu.

Kwa sababu tusizozijua, hadi hivi leo wanafunzi wa darasa la saba hapa Mombasa bado hawajafanya mtihani huu. Yataka wazazi wakimaliza kusoma makala haya wapige mbio hadi kwa afisa wa elimu katika Manispaa ya Mombasa ili wakatake sababu za mtihani huu kuchelewa kiasi hichi. Kama tunavyowaona vijana wetu ni wacheza sana na wapatapo nafasi ya kuacha vitabu huitumia vizuri mno. Huu ndio wakati wa kumsaidia kijana wako apate matokeo ya juu kabisa katika C.P.E. ili apate Shule ya Upili ya Serikali. Iwapo mtoto wako atapata matokeo mabaya katika mtihani huo, basi si mjumbe wala si diwani atakayeweza kukuendea mbio ili kijana wako apate nafasi.

Tokea hapo kazi ya mjumbe au diwani ni kujenga shule nzima au darasa zima sio kutafuta nafasi ya kijana mmoja. Kwani kura moja ya baba au mama wa kijana huyo haimfanyi mtu kuwa mbunge wala diwani. Wote waliochagua wanahaki ya kuhudumiwa bila ya ubaguzi.

RAIS Moi akipokea shada la maua kabla ya kuweka jiwe la msingi katika shule ya ufundi ya Sheikh Zayed mjini Mombasa.
PICHA: KENYA NEWS AGENCY

Dini Ya Kiislamu Inahimiza Sana Uadilifu

NATOWA pongezi zetu kwa makala yalochapichwa katika nakla ya gazetila *COASTWEEK* mnamo tarehe August 20 1982, yalotowa kinaganaga fikra na ukweli ambao wengi katika waislamu walikuwa wa kiuficha kwa sababu mbali mbali ambazo wenyewe wazifahamu. Ni juu ya kila muislamu kutowa fikra zake na maoni yake juu yakila lile ambalo aliona latendeka kombo kuhusu Dini.

Kimya chetu, kwa sababu ya labda uchache wa ujuzi na kuogopa kutajika binafsi kua mwenye kuanza kutoboa siri za walio bora ili kukhofu kupotoka midomo au kupata Laana ya dunia na akhera kwa kusema ati ya sio tuhusu, ndio sisi waislamu tukawa nyuma, kwa kila mambo yetu. Iwapo haki hatuwezi kuikabili na kuisema vile ilivyo, bila ya kuogopa sura au Sharafu ya kujipa. Basi itakuwa vigumu sana kuweza kuwa na umoja na kudai haki yoyote ile inayo husu waislamu au dini yetu.

Dini yetu ya kiislamu mara nyingi imesisitiza ukweli udhihirishwe na kila mtu aujue, iwapo ni mtoto au mtu mzima, amesoma dini au laa. Nihaki ya kila muislamu kujuzwa na yoyote mwenye kujua ukweli wa mambo, vile mambo ya livyo na yatendekavyo. Nayoyote yule mwenye kumiza au kuficha ukweli bila ya kuutangaza kwanjia moja au nyingine, bila shaka mtu huyu ni khain kwa waislamu wote na pia dini. Muislamu wa kweli ni yule mwenye kuutowa bayana ukwelina kila mtu kuufahamu.

Makala ya ndugu Saidi Burhan hayakuficha ukweli wote ule anao ujuwa yeye mwenyewe, na baadhi ya wasilamu wengine ambao walichagua kuuficha kwa sababu zao binafsi, au kama tusemavyo kila mara tuwapo hatuutaki kuukabila ukweli kwa "wowote hao watendaomaovu na mungu wao". Ili tuu kujiepusha na ukweli na kuwacha tuishi tuu vile mambo yanavyo pita bila kujaribu njia yoyote ile kujirakibisha. Ati, Mungu ajua na ndiye mwenye kuhumum, na sisi waislamu ni kuketi tu na kodoa macho, na kusema kichini chini bila kuinua sauti yetu na kusikika kubaini haki ilivyo.

Ndugu Burhan katika makala yake hakuteleza khatua alizotkua ili kurekebisha makosa yalotendwa na huyo alomwita "Walii mwenye damu ya mtume", na wala hakutaja mjadala baina yao, au wafuasi wake ili tujue na kufahamu ukweli zaidi pale ulipo simama. Ndugu Burhan hakusita hata kidogo kubainisha na kumtahadharisha, huyo "Walii" kwa matendo na fikra zake. Hili jambo ama ni sawa au ovu iwapo halikuchunguliwa kwa njia inayofaa na kutiwa kwenye mizani ya akili.

Washauri au Wafausi

Ukweli wa mambo hayo bado haujafahamika, ikiwa ni huyo bado Bwana "Walii mwenye damu ya mtume" au wafuasi wake. Kwani mara nyingi sana utaona kiongozi huwa na washauri au wafuasi wenyefikira na vitendo ahidi ya vile maagizo yao yalivyo. Nasisi bila ya kuchungua humlaumu huyo kiongozi kwa maovu ya wafuasi wenye kujipendelea kujikusanyia mali ya watu kwa matumizi yao binafsi.

Wavamizi kama hao ndio wenye kuleta sifa mbaya kwenye dini na tafauti na kashfa kama hii kwa viongozi. Hata hivyo ni juu ya kiongozi, ijapokua ana kazi nyingi na zito kuangalia na kukagua yale maagizo yake yametekelezwa kama alivyo pendekeza. Akosapo kufanya hivyo, basi hana njia ya kuepuka lawama na jukumu la dunia na kesho Akhera.

Twatambua kua jukumu la tende limepewa wafuasi wenye kujita waadilifu na kutenda yalo sawa, lakini wao ndio walioleta haya mambo ya Ati baadhi hii ni ya Sheikh Abdalla na ile ni ya Mwenye ili tuu kwa manuffaa yao binafsi. Najua mmoja wa watu hawa ambae kwake tende haikupungua tokea mwanzo wa Ramadhani hadi sasa na pia kwa wale waiomuhusu yeye, yaani watu wa ukoo wake. Mtu huyu bi mmoja katika watu wanao tajika mjini Mombasa Mwenye miliki na taslimu nzuri, mtu huyu ndie tende imefutikwa katika ghala yake, lakini ameruzukiwa na udhoofu na umaskini wa roho, na ulafi wa mali ya Uma bila ya kujali adhabu ya kesho Akhera inaymgoja.

Mwenye Enzi Munguatuepushe aayo, Amin.

Ahmed/Rashid — Mombasa.

Vifaa Vyote Viligawanywa Wa Mujibu Wa Quran

Nimesoma barua ya Said Burhan katika *Coastweek* na nikashangazwa kuona kwamba anaona makosa ya watu wengine lakini yake hayaoni. Kuhusiana na huyo walii aliyepata pesa, tende, mazulia na kadhalika, na agawanya kama alivyofanya, basi hivyo ndiyo sawa kwani alifata amri ya Quran tukufu. Maana ilivyo katika Quran ni kwamba, kwanza sadaka huanza kwa watu walio karibu nawe halafu ndiyo ukawapa maskini. Na hao watu waliopata tende, pesa na mazulia ilikuwa ni riziki yao na hao wasiopata hutokezea na hao wasiopata ilikuwa si riziki yao.

Huna haja ya kukasirika kwani haya mambo hutokezea kila mahala. Mwaka juzi ilikuja tende kutoka Iraq ikafikia kwenu na sisi hatukuipata na wala mambo haya hayakuzungumzwa misikitini wala kuandikwa magazetini. Lakini ndugu Said mimi nakupa dawa ya mambo haya kuondoka. Wewe kaza moyo ujifanye mcha Mungu na uwe na moyo wa ibada na mambo hayo yote nawe pia utaletewa huna haja ya kumuonea wivu mtu wa watu. Ikiwa yako ni ya shekhe Abdalla Farsy basi muarifu umwambie ile misikiti uliyosomesha haikupatiwa tende wala mazulia na pesa awaletee nyingi mwaka ujao mufanye haki.

A. A. Mohammed LAMU.

RAIS Moi akipeana kikombe kwa mshindi katika maenyesho ya kilimo ya Mombasa wiki jana.
PICHA: K.N.A.

Wa Kibokoni Tende Hatukuiramba

Kwa hisani yako napenda unichapie haya yangu machache katika gazeti letu la *COASTWEEK*. Mimi nikiwa mkaazi wa hapa Kibokoni Mombasa kwa hakika napenda sana kukuunga mkono kwa dhati yangu, Ama makala yako yote ni ya kweli. Sote hatukula tende, hatukuona mazulia wala mitambo ya maji ya baridi. Nakupa heko bwana Said kusema kweli ni thawabu.

Mariam Ramadhan, Kibokoni, MOMBASA.

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO.

SWAHILI CROSSWORD NO 146

KWENDA KULIA:

1. Moja katika tuzo zinazotolewa na COASTWEEK.
6. Semea, wakilisha
8. Mji katika Tanzania
9. Uteo zaidi ya mmoja.
10. Kabila la pwani Kenya
13. Kwenda kwa miguu na mikono.
16. Neno la kuuliza swali
17. Boma kando ya nyumba
18. Nyumba au sanduku la mnyama.

KWENDA CHINI:

2. Jina jingine la barua kwa wingi.
3. Kubali
4. Tunza angalia mtoto
5. Ndani kwa Kimombo
7. Beda, chukua
11. Ugomvi
12. Kazi
14. Bora nzuri zaidi
15. Vumbua.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 145

1. Abdalla S. Mwazanzale, Sanduku La Posta 83072 Mombasa.
2. Faraj A. Masoud Sanduku La Posta 50 Malindi
3. Siaka Hussein Sanduku La Posta 90581 Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANOI LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 145 —

KWENDA KULIA:
1. KUNGUNI, 5. KA, 6. MWAMBA, 7. RAHA, 8. ANGAZA, 10 IKIWA, 11. TUMA, 15. KINANGO.

KWENDA CHINI:
1. KOMBA, 2. GUMBA, 3. NYARAKA, 4. LA, 5. KAHAWA 9. NYUNI, 12. ADA, 13. LO, 14. CW.



JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindano la Fumbo La Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washinidi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK Limited* Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe September 8, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.